**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Ishirini na Nane – Tarehe 09 Juni, 2021.**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

## I. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

123. MHESHIMIWA HABIB ALI MOHAMED (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Mabaraza ya Miji yana majukumu ya kukusanya mapato tu, bali yanapaswa kusimamia na kutoa ruhusa ya ujenzi katika maeneo mengi nchini ikiwemo Shehia ya Limbani, Mtaa wa Mahaluwa. Hata hivyo kutokana na kutosimamia majukumu yao ipasavyo wananchi wanalazimika kuingia katika migogoro isiyo ya lazima hadi kufikishana Mahakamani kutokana na tatizo la majenzi.

(a) Je, ni upi utaratibu na wajibu wa Baraza la Mji wakati mtu ameomba ruhusa ya kujenga.

(b) Kuna sababu zipi zinazowazuia watendaji wa Mabaraza ya Mji kwenda “field”, kutoa muongozo na kusimamia ujenzi katika hatua za mwanzo ili kuepusha migogoro isiyo ya lazima.

(c) Na kama wanakwenda “field”, kwanini migogoro ya ujenzi inajitokeza mara kwa mara.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

200. MHESHIMIWA ABDALLA ABASI WADI (Jimbo la Nungwi)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa juhudi zake kubwa za kurejesha huduma ya maji hasa katika kijiji cha Nungwi. Pamoja na juhudi hizo, wananchi wa vijiji vya Kigunda, Mwambale, Kilindi na Tazari bado hawapati huduma ya maji safi na salama kwa sababu vipo visima ambavyo vimechimbwa katika vijiji hivyo na pampu zake zimeharibika.

Je, ni lini Serikali itavifanyia matengenezo visima hivyo.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

72. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kwa muda mrefu tumeshuhudia migogoro ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Zanzibar "ZFF" hata baada ya kufanya uchaguzi. Hivi sasa, ZFF haina Mwenyekiti wala Makamo Mwenyekiti, jambo ambalo halileti taswira nzuri kwa soka la Zanzibar, na kupelekea chombo hicho muhimu kufanya maamuzi ya kushangaza ikiwemo kutoa tamko kwamba hakuna timu zitakazoshuka daraja msimu huu.

(a) Je, ni nchi gani inayofuata Sheria za FIFA ambapo timu za nchi hiyo hazishuki daraja baada ya ligi kumalizika.

(b) Je, ni sababu gani za msingi zilizopelekea ZFF kuamua kutoshusha timu daraja.

(c) Je, Serikali haioni kwamba muda umefika wa kuivunja ZFF.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

102. MHESHIMIWA MWANAASHA KHAMIS JUMA (Jimbo la Dimani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Jimbo la Dimani limezungukwa na bahari na wananchi wengi wanajihusisha na kazi ya uvuvi kupata kipato chao. Hata hivyo, wavuvi wengi wanapata changamoto kubwa ya vifaa vya uvuvi ikiwemo boti za kisasa za kuvulia.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wananchi hao kwa kuwapatia boti za kisasa za uvuvi na vifaa vyengine vya kuvulia ili kuongeza kipato na kunufaika na Uchumi wa Buluu.

(b) Katika kufanikisha matokeo bora ya Sera ya Uchumi wa Buluu, Je, Serikali haioni umuhimu wa kuanzisha mfuko maalumu wa kuinua wavuvi wadogo ili wamudu kufanya uvuvi wa kisasa.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

49. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Ilani ya CCM 2020-2025 imesisitiza umuhimu wa kuwaendeleza wafugaji kwa upande wa Tanzania Bara na Zanzibar. Hata hivyo, kwa upande wa Zanzibar shughuli za ufugaji hasa wa ng’ombe na mbuzi zimepungua kulinganisha na miaka 20 iliyopita, hali ambayo imerejesha nyuma sana jitihada za wafugaji.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuendeleza shughuli za ufugaji hapa Zanzibar.

(b) Je, Zanzibar imejitosheleza kwa asilimia ngapi katika upatikanaji wa bidhaa za mifugo kwa nyama na mayai.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

41. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Wananchi wa shehia ya Sizini pamoja na vitongoji vilivyo jirani wanapata tatizo kubwa la mawasiliano takriban mitandao yote ya simu.

Je, ni lini Serikali kupitia Kampuni za Simu itafanya juhudi za kuwaondolea kero hiyo kwa kuwajengea mnara kwenye shehia hiyo.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

134. MHESHIMIWA YAHYA RASHID ABDULLA (Jimbo la Kwahani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Serikali inaandaa Sera mpya ya Elimu ya mwaka 2020 ambayo itachukuwa nafasi ya Sera iliyokuwepo tangu mwaka 2006.

(a) Je, ni kwa kiasi gani jamii imeshirikishwa kutoa maoni yao katika kuandaliwa kwa Sera hiyo.

(b) Je, ni wadau wepi wa Elimu ambao Wizara ilizingatia maoni yao.

(c) Je, ni kwa kiasi gani yaliyotegemewa kutekelezwa katika sera ya zamani yamefanyiwa kazi.

190. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani)

\-

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Katika Skuli ya Msingi Mwambe kuna upungufu mkubwa wa walimu. Tatizo hili limekuwa la muda mrefu na wanafunzi wa maandalizi na msingi wamekuwa wakiongezeka mwaka hadi mwaka.

(a) Je, Waziri umeshawahi kufanya ziara katika Skuli ya Msingi ya Mwambe.

(b) Je, Serikali inawaahidi nini wananchi wa Mwambe katika kulichukulia hatua suala la uhaba wa walimu.

**Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:**

170. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Miongoni mwa maradhi yanayopoteza maisha ya watu wengi hapa Zanzibar ni maradhi yasiyoambukiza.

(a) Je, kwa Zanzibar ni asilimia ngapi ya vifo vinavyotokana na magonjwa yasiyoambukiza kwa mwaka.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza vifo vinavyosababishwa na magonjwa hayo.

**Zanzibar,**
**09 Juni, 2021.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA**